



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO
TAASISI YA CHAKULA NA LISHE TANZANIA



TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU JUMAMOSI TAREHE 27.11.2021

Tunapenda kuwatangazia kuwa mnada wa hadhara wa kuuza vifaa chakavu utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 27.11.2021 kuanzia saa 04.00 asubuhi Makao Makuu ya Taasisi ya Chakula na Lishe 22 Barabara ya Barack Obama na Maabara ya Taasisi iliyopo Mikocheni.

Vifaa chakavu vya aina mbalimbali vitakavyouzwa ni kama vilivyoonyeshwa hapo chini:

- i) Vifaa mbalimbali vya TEHAMA (Personal Computers, Servers, laptop, Scanners, projector, UPS, etc)
- ii) Matairi ya magari
- iii) Samani za aina mbalimbali (Viti, meza, makabati na kadhalika)
- iv) Mabati (used)
- v) Mizani za kupimia uzito
- vi) Vifaa vya maabara
- vii) Vifaa vya Umeme

viii) Vifaa vinginevyo ni (Viyoyozi, jiko,” telephone receiver”, “Water bath” na vifaa vya chuma.

MASHARTI YA MNADA

1. Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo.
2. Atakayetaja bei ya juu kabla ya nyundo kugongwa ndiye atakayeuziwa kifaa.
3. Aliyetaja bei ya juu sio lazima auziwe kama bei hiyo haijafikia bei iliyotarajiwa
4. Mnunuzi atatakiwa kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya vifaa vilivyonunuliwa, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa vifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa.
5. Mnunuzi atatakiwa kuondoa / kuchukua vifaa alivyonunuwa katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
6. Ruhusa ya kuangalia / kukagua vifaa itatolewa kuanzia tarehe 11-26 Novemba, 2021 saa 3.00 asubuhi hadi saa 9.00 alasiri.

**MKURUGENZI MTENDAJI
TAASISI YA CHAKULA NA LISHE TANZANIA (TFNC)**

Mahali Vifaa Vitakapouzwa

Taasisi ya Chakula na Lishe

Barabara ya Barack Obama na Maabara ya Taasisi ya Mikocheni

Dar es salaam